

## **Cheti cha ardhi ya kijiji (fungu la 7 kifungu cha 7)**

### **Maana ya cheti cha ardhi ya kijiji**

- Cheti hiki kinathibitisha mfumo wa ukaaji na utumiaji wa wanakijiji wa ardhi ya kijiji kwa mujibu wa sheria za kimila katika eneo la kijiji.
- Cheti kinabainisha mipaka ya ardhi ya kijiji badala ya hatimiliki za ardhi ya kijiji ambazo zilitolewa kwa baadhi ya Halmashauri za vijiji.
- Hatimiliki za ardhi ya kijiji zilizotolewa kwa baadhi ya Halmashauri za vijiji zitaendelea kutumika kubainisha mipaka ya kijiji hadi hapo cheti cha ardhi ya kijiji kitakapotolewa.
- Cheti cha ardhi ya kijiji kinathibitisha mamlaka ya Halmashauri ya kijiji kusimamia ardhi ya kijiji tofauti na Hatimiliki ya ardhi ya kijiji ambayo ingemaanisha Halmashauri ya kijiji kumiliki ardhi ya kijiji, hivyo kuwanyima fursa wanakijiji kumiliki ardhi kwa mujibu wa sheria.

### **Utoaji wa cheti cha ardhi ya kijiji**

#### **(kanuni ya 37 na 78 na fomu Na. 16 na 16A)**

- Halmashauri ya kijiji inatakiwa ibainishe mipaka ya kijiji na pasiwepo na mgogoro wowote wa mipaka kati ya kijiji na majirani zake. Kijiji kiandae mchoro/ramani ya kijiji kwa ushirikiano na Halmashauri ya Wilaya.
- Halmashauri ya kijiji iwasiliane na Afisa Ardhi wa Wilaya ili aweze kuwaandalia cheti cha ardhi ya kijiji na kukifungulia jalada.
- Kama kijiji kiliwahi kupata Hatimiliki ya kijiji, Afisa ahakikishe kuwa hatimiliki hiyo inarejeshwa kwanza ndipo cheti cha ardhi ya kijiji kitolewe. Aidha, ramani (deed plan) iliyo katika Hatimiliki inaweza kutumika kuandaa cheti cha ardhi ya kijiji iwapo , mipaka ya kijiji haijabadilika.
- Vyeti vigongwe lakiri au muhuri wa Halmashauri kijiji na vishuhudiwe na kusainiwa na Mwenyekiti wa kijiji na Afisa Mtendaji wa kijiji.
- Afisa Ardhi wa wilaya aambatanishe vyeti na barua na kuvituma kwa kamishna wa Ardhi ili vikasainiwe na kuwekewa lakiri. Vikishasainiwa na kamishna, vyeti vitarudishwa wilayani kwa ajili ya kusajiliwa katika Masjala ya Ardhi ya Wilaya, na vitapewa namba ya usajili.
- Vyeti vikishasajiliwa nakala moja itabaki katika Masjala ya Ardhi ya Wilaya, na Halmashauri ya kijiji itakabidhiwa nakala moja ya cheti ili iweze kukitunza katika Masjala ya ardhi ya kijiji.

- Baada ya kupata cheti cha ardhi ya kijiji ndipo Halmashauri ya kijiji inapokuwa na mamlaka rasmi ya kusmamia ardhi ya kijiji.
- Endapo mipaka ya ardhi unarekebishwa au kubadilishwa ni wajibu wa Halmashauri ya kijiji kupitia kwa Afisa ardhi wa Wilaya kumpelekea kamshna cheti cha Ardhi ya kijiji ili athibitishwe kwenye cheti mabadiliko hayo.